

JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MANISPAA YA TABORA

SHULE YA SEKONDARI ISEVYA,
S. L. P 191,
TABORA.

TAREHE...../...../20....

Kumb. Na. **ISS/F.I/SEL/2021**

Ndg,

**YAH: KUTEULIWA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI YA SERIKALI ISEVYA
TABORA KIDATO CHA KWANZA MWAKA 2021.**

Ninafuraha kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na Shule ya Sekondari ya kutwa ya Serikali Isevya kidato cha kwanza (**Form I**) Mwaka **2021**. Napenda kukupongeza kwa kupata nafasi hii ya kuendelea na masomo ya Sekondari ambayo Taifa limekupa kutokana na juhudi zako.

Ni matumaini yangu kwamba utaendelea na juhudi hiyo na hata zaidi kulihakikishia Taifa kuwa nafasi uliyopewa utaithamini na kwamba utaitumia vema kujiendeleza kwa faida yako na Taifa lako kwa ujumla.

Utafanikiwa kufikia lengo hilo iwapo tu utafanya shughuli zako kwa juhudi, maarifa na nidhamu ndani na nje ya darasa kama utakavyoelekezwa na walezi wako kwa taratibu zilizowekwa na Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na mafunzo ya ufundi na **TAMISEMI**.

Shule itafunguliwa tarehe **04/01/2021**, fika shuleni siku hiyo saa mbili asubuhi bila kukosa, kwa ajili ya maelekezo ya awali.

Mwisho, nakutakia mafanikio mema na maisha ya raha Shuleni.

.....

MKUU WA SHULE

MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA ILI KUJIUNGA NA SHULE HII

Unatakiwa kutimiza mambo yafuatayo kabla ya kujiunga na shule hii.

A. SARE YA SHULE (MAVAZI YA HESHIMA)

WASICHANA

- i. Sketi mbili za rangi ya **zambarao** ndefu zinazofunika magoti zenye rinda box inchi $1\frac{1}{2}$, Sketi unashona mwenyewe.
- ii. Blauzi (shati) mbili nyeupe za kitambaa cha tetron mikono mifupi zisizo na urembo.
- iii. Viatu Vyeusi vyenye visigino vifupi (visivyogonga) na soksi za kike ndefu nyeupe.
- iv. Kwa Waislamu: Sketi ndefu zinazofunika miguu yao, shati (blauzi) zenye mikono mirefu pamoja na shungi nyeupe zinazofunika vifua vyao (shungi zisiwe na urembo)
- v. T-shirt ya mikono mifupi ya rangi ya njano
- vi. Tai inayofanana na sketi
- vii. Sketi nyeusi kwa ajili ya kufanyia kazi na michezo
- viii. Sweta ya rangi ya zambarao

NB: Tunashauri mwanafunzi awe na sare zaidi ya moja na azitunze kwa usafi wa hali ya juu

WAVULANA

- i. Suruali mbili za rangi ya zambarao suruali zote unashona mwenyewe (mzazi) mshono wenye marinda matatu mbele kila upande na mifuko miwili, mfuko mmoja nyuma upande wa kulia upana wa chini miguuni uwe usiobana (**MODO HAZIRUHUSIWI**)
- ii. Shati mbili nyeupe (tetron) mikono mifupi zisizobana
- iii. Viatu vyeusi (visivyogonga) vyenye visigino vifupi
- iv. Soksi nyeusi
- v. Nguo za michezo – bukta zisizobana za rangi ya bluu, na T-shirt ya mikono mifupi rangi ya njano
- vi. Tai inayofanana na suruali

B. URAIA

Aje na nakala ya cheti cha kuzaliwa

C. MAHITAJI YA MWANAFUNZI

1. Madaftari makubwa 15 au zaidi
2. Kalamu za wino mbili au zaidi
3. Kalamu za risasi, kifutio, rula na mathematical set

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI, TEKNOLOJIA, MAFUNZO YA UFUNDI NA TAMISEMI

UTANGULIZI

Sheria na kanuni muhimu za shule hii

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia, Mafunzo ya Ufundi na **TAMISEMI**, yenye dhamana ya elimu nchini na Ofisi ya Rais – **TAMISEMI** yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa Elimu. Unatakiwa kuzingatiam mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni:

- a. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima;
- b. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima;
- c. Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (preparation);
- d. Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa;
- e. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
- f. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
- g. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
- h. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote; na
- i. Kutunza mali za UMMA

MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA SHULE MOJA KWA MOJA

1. Wizi
2. Uasherati na ushoga
3. Ubakaji
4. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevywa kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kuberi n.k
5. Kupigana au kupiga
6. Kudharau Bendera ya Taifa
7. Kuharibu kwa makusudi mali ya Umma
8. Kuoa au kuolewa
9. Kutoa mimba
10. Kuwa mjamzito au kupata mimba
11. Kugoma, kuchochea au kuongoza au kushiriki kuvunja amani na usalama wa shule au watu
12. Kukataa adhabu kwa makusudi
13. Kuwa na simu ya mkononi

14. Kujiachisha shule mwenyewe.

NB: Kanuni na sheria hizi zinaweza kurekebisha kutokana na mabadiliko yanayojitokeza au mahitaji. Ni haki ya shule na wizara tu kufanya mabadiliko

MIPAKA YA SHULE

- i. Shule inayo mipaka inayofahamika kwa jumuiya yote
- ii. Wanafunzi hawaruhusiwi kutoka nje ya shule yaani nje ya mipaka hiyo isipokuwa kwa kibali maalum
- iii. Saa za kutoka nje ya mipaka ya shule zinaonyweshwa katika ratiba ya kila siku. Wanafunzi wanatakiwa kufika shuleni kwa wakati uliopangwa
- iv. Kibali cha kwenda nje ya wilaya/mkoa atatoa mkuu wa shule au makamu wake

USAFI

Usafi wa mwanafunzi unasisitizwa kama sehemu ya maisha yao ya kila siku pamoja na usafi wa madarasani, ofisi, vyoo na maeneo yote ya shule kwa ujumla. Uharibifu na uchafuzi wa mazingira hauruhusiwi kabisa katika shule hii.

MAANDALIO YA JIONI/NYUMBANI (HOMEWORK)

- i. Ni muhimu wanafunzi kufanya maandalio ya jioni kujiandaa na siku inayofuata kimasomo
- ii. Ili kufanikisha utaratibu huu walimu wa masomo watatoa kazi na kuhakikisha kuwa kazi hizo zimefanywa, hivyo kazi maalumu zitatolewa na patakuwepo pia utaratibu wa kuzipima na kuzifuatilia kikamilifu

KUWAHI

- i. Wanafunzi wanapaswa kuthamini muda
- ii. Wanafunzi wanatakiwa kuwahi katika shughuli zote za shule kama zilivyopangwa katika ratiba ya kila siku. Wachelewaji watakaofahamika watachukuliwa hatua.
- iii. Wanafunzi wanatakiwa kuwahi wanaposikia wito wa dharula
- iv. Shule ina chombo (kengele) kinachowajulisha wanafunzi muda wanaotakiwa kwa shughuli mbalimbali, hivyo inapopigwa kengele wanapaswa kuwahi kusikiliza wanachoitiwa.
- v. Wanafunzi wanatakiwa kufika shuleni kwa tarehe zilizopangwa wakati wa likizo fupi au ndefu watakaokiuka hatua za kinidhamu zitachukuliwa dhidi yao.
- vi. Wanafunzi hawaruhusiwi kutoka eneo la shule kabla ya muda wa masomo kuisha

ZINGATIA

- Shule ina sare inayojulikana kwa wanafunzi na jumuiya nzima na ipo katika mshono unaokubalika kulingana na heshima inayosisitizwa na taifa na maadili ya jamii.

KUMBUKA SARE NI VAZI LA SHULE NA RASMI LIHESHIMU.

Mambo mengine muhimu yanayopaswa kukamilishwa shuleni na mwanafunzi.

- (i) Medical Examination Form ambayo itajazwa na mganga mkuu wa Hospitali ya Serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa Shule mara utakaporipoti shuleni .
 - (ii) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.
 - (iii) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelezo mengine yatakayotolewa na shule.
- ❖ Tafadhali, soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

Karibu sana katika shule hii.

.....

MKUU WA SHULE

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

**MINISTRY OF EDUCATION, SCIENCE, TECHNOLOGY AND VOCATIONAL
TRAINING**

FORM FOR MEDICAL EXAMINATION

To be completed by a medical Officer in respect of all Form I and Form V entrants.

Pupil's full name.....

Age/Years.....Sex.....

Blood found (red and White).....

Stool examination:

Urinalysis:

Venereal Diseases test:

T.B. test:.....

Eye Test:

Ears:.....

Chest:.....

Spleen:.....

Abdomen:.....

Urine for Pregnant:.....

ADDITIONALL INFORMATION (If any) e.g. Physical defects, impairment(s) e.g. arm, leg etc.
infection chronic or family disease etc.

.....

I certify that the above is fit to pursue further education as stated above.

Signature:.....

Designation:.....

Station:.....Date:.....

Official Stamp:

FORM NO.2

A: AHADI YA MZAZI:

Mimi..... (jina kamili) ambaye ni mzazi/mlezi

wa.....Kidato cha
Nimeyasoma maagizo haya na kuyaelewa vema. Nimekubali mwanangu ajiunge na shule hii. Naahidi kwamba nitashirikiana na uongozi wa shule katika kumpatia Mwanangu malezi bora na nitatoa msaada kadri ya uwezo wangu nitakapotakiwa kufanya hivyo. Ninaahidi kwamba nitatekeleza yote yaliyotajwa kwenye barua hii.

Sahihi ya Mzazi/Mlezi.....

Anuani kamili.....

Simu:.....

Tarehe:.....

B: AHADI YA MWANAFUNZI

Mimi..... (jina kamili) ambaye ni mwanafunzi, nimeyasoma maagizo haya na kuyaelewa, ninakubali nafasi niliyopewa ya kujiunga na shule hii.

Ninaelewa wazi kwamba shuleni ni mahali pa kujifunza na mimi nina nia ya kujifunza. Ninaelewa pia kuwa nafasi hii niliyopewa ni dhamana, hivyo naahidi mbele ya wazazi/walezi wangu ya kwamba nitaitumia vema nafasi hii kwa kushirikiana na uongozi wa shule kutimiza na kutekeleza yale yote yaliyo katika maagizo haya. Nitatii na kufuata sheria za shule wakati wote. Naahidi pia kufanya bidii katika masomo yangu na kuwa mfano mwema kwa wenzangu wakati wote. Naahidi pia kufanya bidii katika masomo yangu na kuwa mfano mwema kwa wanafunzi wenzangu wakati wote.

Sahihi ya mwanafunzi.....

Tarehe.....

Shahidi (Kiongozi wa Serikali ya Mtaa/ Kijiji)

Jina kamili.....

Sahihi.....

Tarehe.....

FORM NO.3

SHULE YA SEKONDARI YA ISEVYA

TAARIFA MUHIMU ZA MWANAFUNZI

1. JINA LA MWANAFUNZI.....
2. KABILA.....
3. TAREHE YA KUZALIWA.....MWEZI.....MWAKA.....
4. AMEZALIWA KATIKA WILAYA YA.....
MKOA WA.....
5. DINI.....DHEHEBU.....
6. JINA LA MZAZI/MLEZI.....
(Ikiwa mzazi amefariki andika jina la mlezi hapa)
7. ANWANI YA MZAZI/MLEZI.....
8. (KIJIJI)(TARAFU)(WILAYA)(MKOA)
Na. ya simu.....
9. KAZI YA BABA/MLEZI.....
10. KAZI YA MAMA.....
11. Afya ya mwanafunzi (kama ana ugonjwa unaohitaji uangalizi uandikwe: Taja udhaifu wowote wa mwili au afya yake na uambatanishe cheti cha Daktari).
.....
.....
12. Majina ya Ndugu wengine wanaohusika na malezi ya huyu mwanafunzi (**matatu tu**) na anuani zao kamili:
 - (a) Ndugu.....
Uhusiano.....
Anuani.....
Na. ya simu
 - (b) Ndugu.....
Uhusiano.....
Anuani.....
Na. ya simu
 - (c) Ndugu.....
Uhusiano.....
Anuani.....
Na. ya simu

.....

SAHIHI YA MWANAFUNZI

TAREHE:.....

SAHIHI YA MZAZI/MLEZI

TAREHE:.....